# MZALENDO

## Ukarabati wa Reli ya Kati umekuja wakati mwafaka

MWISHONI mwa wiki hii, serikali ilitangaza kutenga zaidi ya sh. bilioni 500 kugharimia ukarabati wa Reli ya Kati kutoka Dar es Salaam hadi Isaka kuelekea Zambia.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alitoa taarifa hiyo katika kikao maalumu cha kutambulisha utekelezaji wa awamu ya pili ya ukarabati wa reli hiyo kwa viongozi wa mkoa na wawakilishi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Kwa mujibu wa Malima ukarabati huo unahusisha madaraja, vituo vya reli, vivuko vya magari na uboreshaji wa nyenzo za reli na serikali imedhamiria kufufua reli hiyo kwa kiwango cha kisasa kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Alisisitiza kwamba ofisi yake ipo tayari kushirikiana na TRC na mamlaka zote zinazohusika kuhakikisha ukarabati huo unatekelezwa kwa ubora, kukamilika kwa wakati na kuharakisha maendeleo ya Mkoa wa Morogoro na taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Uhandisi wa TRC, Mhandisi Joseph Kilasara, alisema utekelezaji wa mradi huo, utaenda sanjari na teknolojia mpya itakayowezesha magari ya reli kusafiri kwa kasi zaidi na kwa usalama mkubwa.

Alisema marekebisho hayo yatapunguza muda wa safari, kati ya Dar es Salaam na mikoa ya kati, jambo ambalo litavutia wawekezaji wengi zaidi katika ukanda huo, ambapo baadhi ya wananchi wa mkoa huo, walisema reli hiyo ni kiungo muhimu kwa biashara na shughuli za kila siku.

Tunaipongeza serikali kwa uamuzi wa kutenga kiasi hicho cha fedha kukarabati miundombinu ya reli kutoka Dar es Salaan hadi Isaka, kwa kuwa itawezesha treni kupita kwa kasi na hivyo kupunguza muda wa safari.

Aidha ukarabati huo, utaongeza ufanisi wa reli na hivyo kuongeza idadi ya abiria na mizigo kutokana na uboreshaji wa miundombinu hiyo muhimu katika sekta ya usafirishaji nchini.

Ieleweke kuwa usafiri wa treni ni moja ya vyombo vya usafiri vinavyotegemewa na wananchi walio wengi kutokana na unafuu, usalama na uhakika wa safari kutoka eneo moja hadi lingine huku ikiwa na uwezo mkubwa wa kusafirisha shehena kubwa za bidhaa.

Ni hatua nzuri hasa ikizingatiwa kwamba tayari mtandao wa reli nchini umeendelea kuimarishwa hasa baada ya ujio wa treni ya mwendo kasi ya SGR inayotoa huduma zake kati ya Dar es Salaam hadi Dodoma.

Pia tayari TRC imeanza majaribio ya usafirishaji wa shehena za mizigo kwa kutumia treni ya mwendo kasi kati ya Dar es Salaam hadi Dodoma, hatua ambayo imefungua ukurasa mpya wa mafanikio ya huduma za reli nchini.

Hivyo, uamuzi wa ukarabati wa reli kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Isaka umekuja wakati mwafaka kutokana na mahitaji ya miundombinu ya reli katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi na wafanyabiashara kutoka nchi jirani.

Ni matarajio yetu kwamba ukarabati huo, utafanyika kwa viwango, ubora na kasi ili kuongeza thamani ya miundombinu ya reli, ambayo ni tegemeo kubwa kwa wananchi na wafanyabiashara kutokana na unafuu, uhakika na usalama wa chombo hicho.

**Uhuru Publications Limited (UPL)**
S.L.P. 9221, Dar es Salaam
Makao Mkuu: Mtaa wa Lumumba Mkabala na Shule ya Msingi Mnazi Mmoja
Chumba cha Habari:
+255-739 957 882/FAX: 2183780
email: uhurunews@yahoo.com
uhuruadvert@gmail.com
uhurumakala@gmail.com

Kaimu Mhariri Mtendaji: ____________ 0784 - 333186
Naibu Mhariri Mtendaji: ____________ 0784 - 599717
Mhariri wa Habari: ____________ 0713 - 117177
Mhariri wa Makala: ____________ 0754 - 305135
Mhariri wa Michezo: ____________ 0718 - 611700

IDARA YA BIASHARA
Meneja Biashara: ____________ 0683 - 378522
Meneja Matangazo: ____________ 0765 - 142207
Kaimu Meneja Mauzo na Usambazaji: ____________ 0715 - 313263

UHURU FM (PMCL)
uhurufmnews@gmail.com
Kaimu Mkurugenzi Uhuru FM: ____________ 0765 - 383757
Kaimu Mhariri Mkuu Uhuru FM: ____________ 0713 - 248640

CamScanner